

MSTARI WA MAOMBI



...?...Ni wangapi wamehudhuria mikutano yangu hapo kabla? Hebu tuone mkono wako. Kabla ya mkutano huu hapa, kabla ya Evansville? Vema. Usiku wa leo, kwa kuwa nimepwelewa na sauti, nisingeweza kuhubiri, ninashukuru kwamba nina karama nyingine. Mnaona? Haihitaji mahubiri yoyote. Hebu, Mungu anaweza kuhubiri. Hiyo ni kweli? Acha Mungu ahubiri, chochote anachotaka kuhubiri usiku wa leo, hiyo ndiyo sababu aliniacha nipwelewe na sauti.

² Huyu hapa mama amesimama, sijawahi kumwona maishani mwangu, sijui lolote kumhusu. Hatufahamiani, sivyo? Hatufahamiani? Hatujawahi kuonana? Kwa hiyo, kama mwanamke huyu yuko hapa, sijawahi kumwona, tumeachana kwa miaka mingi kwa umri, labda tulilelewa umbali wa maili kadhaa, bali Mungu anamjua. Hivi hamuamini hilo? Yeye ananijua.

³ Sasa, kwa ono, Yeye anaweza kuniambia shida yake. Mnaamini hilo? Hilo ni hili: Ikiwa Yesu amefufuka katika wafu, kama Yesu angekuwa amesimama hapa, Yeye angejua shida yake, sivyo? Naye alisema, “Mambo nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya.” Hiyo ni kweli? Vema, tunamshukuru kwa ajili ya jambo hilo. Nasi tunajua ya kwamba Yeye yupo hapa, na atafanya yale hasa Yeye aliyosema atafanya.

⁴ Sasa, nataka kuzungumza naye, kwa dakika moja tu, kama alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, kuwasiliana na roho yake. Kuna mtu yeyote hapa anayemjua mwanamke huyu? Basi mnajua ana shida gani. Basi kama Mungu Mwenyezi atafunua kwa ono shida ya mwanamke huyu, basi mtamkubali Yeye kama Mponyaji wenu? Mtafanya hivyo? Wangapi watafanya hivyo? Inua mkono wako. Useme, “Ninaliamini.” Ninataka kuzungumza naye.

⁵ Mimi ni ndugu yako, dada. Sikujui wewe, lakini wakati Yesu alipozungumza na mwanamke kisimani, haikuchukua muda mrefu sana mpaka alipopata kujua shida yake ilikuwa ni nini. Alikuwa na waume watano, hiyo ilikuwa ndiyo shida yake. Wako huenda ukawa ni uvimbe, ugonjwa wa kibofu nyongo, sijui, labda kansa, sijui, bali Yeye anajua. Na kama anaweza, katika nguvu Zake, kufunua shida yako, utakubali uponyaji wako? Utafanya hivyo? Utakubali. Uh-huh. Unaamini ninaweza kufanya jambo hili kupitia Yesu Kristo?

⁶ Si kwa ajili yako mwenyewe hasa. Hilo lilikushtusha, sivyo? Ninawaona wavulana wawili, ni wazee, kwa hiyo ni ndugu zako. Na mmoja wao yuko karibu kufanyiwa upasuaji, ni kwa ajili ya henia. Na huyo mwingine ana ugonjwa wa moyo, na namna

fulani ya kikohozi, kikohozi cha pumu. Wewe ni Mkristo, lakini hakuna hata mmoja wao ni Wakristo, unaiombea nafsi yao. Hiyo ni kweli?

7 Hivi hayo, yale yaliyosemwa, ni kweli? Huyu alikuwa ni mimi nikinong'ona, bali ilikuwa ni Yeye akinena. Unaamini utapokea ulichoomba?

8 Kusanyiko lingeweza kusikia hayo? Kama ungeweza, inua mkono wako. Vema. Sikujua tu ni kiasi gani. . . Nilipotoka humu jengoni dakika chache zilizopita, nisingeweza kunong'ona, na kwa hiyo naja hapa kwa imani. Mnaona? Lakini, Yeye yupo hapa.

Sasa njoo hapa kwa dakika moja tu.

9 Baba yetu wa Mbinguni, Wewe unajua hali ya mwanamke huyu, shauku ya moyo wake, ninaomba ya kwamba utatujalia. Jalia apokee tu kile kilichomleta hapa. Basi mikono yangu imewekwa juu yake, kama mtumishi Wako, ninaomba baraka hii, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

10 Mungu akubariki, dada. Yeye Ambaye angeweza kuniambia *kilichokuwa* maishani, anaweza kuniambia kile *kitakachokuwa* maishani. Wewe nenda ukiamini tu yale uliyosikia, utapokea tu yale unayoamini. Mungu akubariki.

11 Hebu tuseme, "Amina." Hebu tuseme, "Bwana asifiwe." *Mungu* ni "kitu cha kuabudiwa." Mungu anajua mambo yote, kwa hiyo Yeye kamwe hatuachi, wala hatupungukii.

12 Ni wangapi huko nje wasio na kadi ya maombi na wanataka Mungu awaponye? Inua mkono wako. Inua tu mkono wako, useme, "Ninataka Mungu aniponye." Mnaomba. Ninawathamini. Mna imani. Ninajua Mungu atawasaidia, na atawaponya.

13 U hali gani, bwana? Nadhani mimi na wewe hatufahamiani. Naam, bwana. Hujawahi kuniona hapo kabla? Vema. Wanapata sauti yako kwenye hiyo maikrofoni, pale. Na, lakini kama hatujawahi kuonana hapo kabla, hatujawasiliana maishani, hata hivyo Mungu anatujua sote wawili, sivyo? Anatujua. Vema, Yeye anaweza kunifunulia shida yako ni nini. Na basi kama anaweza kufunua shida yako, unajua ya kwamba Jambo fulani linatukia kwa sababu ni Malaika wa Bwana.

14 Hata hivyo, sijui ni kwa nini Yeye aliniacha nipwelewe na sauti, ni kwa kusudi fulani, hakika, ndivyo ilivyo. Labda kunizuia kuhubiri, labda kunizuia kidogo tu, ninaenda kama nyumba inayowaka moto, hana budi kunipunguzia mwendo mara moja moja. [Ndugu anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Unafanya hivyo? Shida ile ile. Vema, mara nyingi Mungu inambidi, wakati mwingine, kutuleta mahali ambapo tunaweza kumtambua. Hiyo ni kweli.

15 Una ninii, una namna fulani ya ugonjwa wa figo. Hiyo si ni kweli? Halafu una ugonjwa wa moyo. [Ndugu huyo

anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Naam, bwana. Naam. Naam, bwana. Naam, bwana. Na zaidi ya hayo yote, moja ya mambo makuu sana unayohitaji ni Yesu Kristo awe Mwokozi wako. Naam, bwana. Hujaokoka bado. Umeuahirisha kwa muda mrefu, sivyo, baba? Nywele zinaingia mvi, zinaingia theluji kwa ajili ya Umilele. Amekuwa mwema kwako, sivyo? Unataka kumkubali sasa? Hali yako, unataka kumkubali? Mungu akubariki, basi. Njoo hapa.

¹⁶ Baba wa Mbinguni, samehe kila dhambi, tujalie, usiku wa leo, mateso ya mwili wake na yaondoke.

¹⁷ Ewe pepo, ninakulaani, katika Jina la Yesu, toka ndani yake!

¹⁸ Jalia mtu huyu aende katika amani, na awe mzima. Kwa ajili ya utukufu wa Mungu tunaomba, katika Jina la Kristo.

¹⁹ Angalia hapa, ndugu yangu, dhambi zako zimesamehewa, utapona, nawe utaishi maisha tofauti sasa. Nenda ukajiunge na kanisa zuri la Injili yote, kisha upokee ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mungu akubariki.

Sasa hebu na tuseme, “Bwana asifiwe.”

²⁰ Unaniamini kwa moyo wako wote, dada? Kama Mungu atanifunulia, hapa, kilicho shida yako, utakubali uponyaji wako? Ulikuwa umeketi pale ukiomba. Hayo ni mawasiliano tu. Unaamini mimi ni mtumishi wa Mungu? Una henia. Hiyo si ni kweli? Unaamini umeponywa sasa? Amina. Mungu akubariki.

²¹ U hali gani, mama? Una mtoto mchanga hapo, naona, msichana mdogo, mgonjwa sana. Unaamini ya kwamba mimi ni mtumishi wa Mungu? Unaamini ya kwamba Mungu yuko tayari kumponya mtoto huyo? Sasa, siwezi kuzungumza vizuri sana, kwa hiyo sina budi kuona ono. Na kupitia hilo, kama Mungu atafunua hali ya mtoto huyu mchanga, chanzo chake, ama tiba yake, kama anajua ni kitu gani kilichomfanya mgonjwa, hakika Yeye anaweza kujua jinsi ya kuuponya, sivyo? Kama anajua yaliyokuwako, Yeye anajua yatakayokuwako, sivyo? Sikuangalii, unaona, kwa kuwa naona ni huyu mtoto mchanga.

²² Alaaniwe ibilisi aliyefanya hivi! Mtoto huyu mchanga amerithi ugonjwa ambao umepokezanwa, ambao ni ugonjwa wa kijamii ambao umemwambukiza huyu mtoto mchanga, nao umesababisha tatizo hili. Hiyo si ni kweli? Naam. Hivyo ndivyo ilivyo. Unaamini Mungu atauponya? Mlete hapa kwangu.

²³ Bwana, ninaweka mikono juu ya mtoto huyu mchanga huku nikijua atakufa, hakika, usipomsaidia. Ninapoweka mikono yangu juu yake, ninambariki huyu mtoto mdogo, ninakuomba umponye. Roho Wako na aje juu yake, nguvu za Mungu na zimfunike mtoto huyu mchanga, pia Nuru ya Mungu na iangaze maishani mwake. Huyu, haiwezi kusaidia, na jalia aishi, ninapombariki, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake. Kwa ajili ya utukufu Wako, Bwana, naomba. Amina.

24 Dada, naweza kuzungumza nawe? Loo, naam. Niliona kitu cheusi juu ya huyo mtoto mchanga...?...kutoka kwa huyo mtoto. Kwa hiyo, amini...?...[Dada huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Vema. Ninataka kusikia kutoka kwako. Ninataka kusikia kutoka kwako. Mungu akubariki. Ninaamini huyo mtoto mchanga atapona. Nenda, amini...?...Mungu akubariki.

25 Kile sayansi ya tiba haiwezi kupata, Mungu anajua. Unaamini hilo? Jambo pekee wanalojua, huyo mtoto mchanga aliteseka, lakini kabla hajateseka, ilibidi pawe na kitu cha kuusababisha. Mungu, Ambaye ni mkuu, anajua mambo yote. Vema.

Njoo, bwana.

26 Loo, kumbe. Yalikuwa ni mahangaiko yako juu ya huyo mtoto mchanga, niliona Nuru ile ikining'inia juu yako, unaona. Nimembariki huyu mtoto mchanga katika Jina la Kristo. Ni wa dada yako. Aminini, nyote wawili. Nawe ndugu, amini jambo lilo hilo kwa moyo wako wote kwamba Mungu atamjalia huyo mtoto mchanga kupona, mtaliona. Baraka za Mungu ziko juu yake. Katika saa sabini na mbili zijazo, mtaona badiliko kubwa sana katika mtoto huyo, itakuwa ni kimiujiza...?...

27 Bwana, uniamini? Mimi ni ndugu yenu tu, bali Yeye anayezungumza kwenye jukwaa hili ni Bwana wenu. Ninaona meza ikija kati yetu, sasa meza inaondolewa nawe unaiondokea. Lakini, kuna kitu fulani, ni—ni tumbo, kidonda tumboni. Je, hiyo ni kweli? Na inaonekana kuna jambo geni kukuhusu. Hebu kidogo. Ninaona unapiga magoti na kuomba huku mikono yako imeinuliwa hewani kuhusu jambo fulani, upate afya, la, sivyo, ni kumpokea Roho Mtakatifu. Huo ndio unaotafuta, sivyo? Hiyo ni kweli? Njoo hapa.

28 Mungu, jalia aupokee, katika Jina la Mwanao, Yesu Kristo. Jalia, Baba wa Mbinguni, kwamba ataupokea, na aponywe, kupitia Jina la Yesu. Amina.

29 Mungu akubariki, ndugu, uponywe na umpokee Roho Mtakatifu, katika Jina la Yesu Kristo.

Njoo, mama.

30 Iweni na kicho, kila mtu, tafadhalini.

31 Unalia nini, bwana? Je, uniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Kama Mungu ataniambia ni shida gani, ungekubali uponyaji wako? Simama kwa miguu yako kwa dakika moja. Roho nyingi sana hapo. Nitazame kama mtumishi wa Mungu. Unaugua TB. Hiyo si ni kweli? Umeponywa. Yesu Kristo anakuponya, naomba uponywe.

32 Mwaminini Mungu.

33 Amini tu. Si lazima uwe hapa juu. Inakubidi kumwamini Mungu. Huna haja ya kuwa hapa juu, amini tu, amini tu.

34 Wewe ndiye mgonjwa, mama? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Hatufahamiani? Hatufahamiani. Uliniona miaka minane iliyopita nilipokuwa hapa. Mungu akubariki. Hapana shaka wewe ni mwuguzi, wewe huvaa nguo nyeupe, na viatu vyeupe, soksi nyeupe, unawahudumia wagonjwa. Nawe una u—ugonjwa wa wasiwasi unaokusumbua, ugonjwa wa kisukari. Hiyo si ni kweli? Njoo hapa. Je, mambo hayo ni kweli? Kama Mungu angeweza kukuponya kitu kingine katika ule mkutano mwingine, hivi hawezi kukuponya huu sasa?

Inamisheni tu vichwa vyenu.

35 Mwenyezi Mungu, ninaweka mikono yangu juu ya mwanamke huyu, nikijua ya kwamba sasa hivi Wewe umesimama hapa. Nami naomba ya kwamba nguvu za Mungu zilizomfufua Yesu kutoka kaburini, zimjalie uponyaji wake sasa hivi. Ninakemea ugonjwa huu, ninaombea uponyaji wake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

36 Dada yangu mpendwa, nenda zako ukishangilia, ukimshukuru Mungu. Utakuwa mzima. Mungu akubariki.

37 Hebu tuseme, “Mungu na ashukuriwe.”

38 Inamisha kichwa chako, ukiweza, ni mtu aliye kiziwi. Hebu kila kichwa kiinamishwe.

39 Bwana, uturehemu. Jalia, Bwana, uponyaji wa mtu huyu, anayekuja Kwako kwa unyenyekevu. Jalia nguvu za Mungu ziupige mwili wake na kumfanya mzima kabisa. Tujalie, Bwana. Shetani alifanya uovu huu. Ninadai ushindi juu yake, katika Jina la Yesu Kristo, jalia atoke ndani yake!

40 Umekuwa hivi kwa muda gani? [Dada huyo anasema, “Ati ni muda gani nimekuwa...? Kwa miaka saba.”—Mh.] Unajua hata kilichotukia hapa? [“Ndiyo.”] Waweza kunisikia, sasa? [“Ndiyo, ninaweza kusikia kutoka upande *ule*.”] Unaweza kunisikia sasa? [“Loo, ndiyo, ninaweza.”] Unaweza? Sema, “Bwana asifiwe.” [“Bwana asifiwe.”] Umeponywa. Hili ndilo sikio lako lisilosikia lililoponywa. Sema, “Bwana asifiwe.” [“Bwana asifiwe.”] “Nampenda Yesu.” [“Nampenda Yesu.”] “Amina.” [“Amina.”] Wewe ni mzima. Ulikuwa na shida kidogo na...? [“Naam.”] Hiyo si ni kweli? [“Naam.”] Nilifanya hivyo tu ili kwamba iichochee imani yako. Huo umekwisha, pia, sasa. Nenda zako ukishangilia, na uwe mzima.

41 Mnampenda? Semeni, “Amina.” Yeye ni wa ajabu.

42 Dada Wood, huyo hapo karibu nawe, tena. Uh-huh. Sijui una shida gani. Kwa nini isiwe ni sasa, Dada Wood? Ukubali sasa. Mwamini Yeye kwa moyo wako wote. Jinsi imani yako itakavyoivuta pale!

43 Unaamini, bwana? Hii hatufahamiani? Sikujui, bali Mungu anakujua.

44 Ninataka kuliuliza kusanyiko...Maono hudhoofisha. Bwana asingeweza...?...Je, mnatambua ya kwamba Danieli aliona ono moja wala asingeweza...?...kichwa chake kwa siku kadhaa. Nyote mnajua jambo hilo.

45 Mungu anamjua mtu huyu, simjui. Hatufahamiani kabisa, lakini Mungu anajua yote kumhusu, Yeye anajua yote kunihusu mimi. Kama nimeshuhudia ile kweli, kama Yesu Kristo angekuwa amesimama hapa, Yeye angeweza kujua shida yake, aseme ni kitu gani kinachomsumbua. Lakini kuhusu kumponya, Yesu tayari amemponya wakati alipokufa pale Kalvari. Imani ya mtu huyu...Na hiyo ndiyo sababu yuko hapa, ni kupata imani zaidi kumwamini Mungu. Haleluya!

46 Niangalie mimi, bwana. Sababu yangu kusema hivyo, maana halisi, ninawatakeni nyote mfahamu: Eliya alimwambia Yehoshafati, na hao wengine, pia, "Kama si kwamba nilimheshimu Yehoshafati, hata nisingekuangalia." Petro na Yohana walisema, "Tutazame sisi." Kwa maneno mengine, ni kuvutia usikivu.

47 Sasa, kama Mungu anaweza kukusaidia kwa kufunua shida yako, ama chochote anachotaka kufunua,...?...je, utamkubali Yesu kama Mponyaji wako?

48 Sasa huyo mtu ananiondokea. Ninaona nyumba, nyeupe. Ni ugonjwa wa tumbo, ugonjwa wa tumbo ulio ndani ya mtu huyo, tumbo lenye vidonda vilivyosababishwa na ugonjwa wa wasiwasi. Umerudi nyuma kabisa.

49 Hiyo ni kweli, bwana? Kama hiyo ni kweli, waweza kuinua mkono wako? Sasa, kama Mungu anajua...Lolote alilosema, hilo ni kweli, sivyo? Sikujui. Kama nikizungumza nawe dakika chache zaidi—dakika chache zaidi ingeendelea, kimsingi sababu ya yeye kusimama hapo, ama kitu kingine. Ninapozungumza na mtu, basi hilo linatukia. Unaamini hilo? Je, kusanyiko linaamini hilo? Hebu nizungumze na mtu huyo kidogo tu. Endelea tu kuangalia huku. Mwamini Yeye kwa moyo wako wote.

50 La, ono lilikuwa hapa. Ilikuwa ni kitu gani? Kulikuwa na shida gani na sehemu ya katikati *hapa*? Jambo fulani kuhusu kula ama *kitu fulani* kuhusu tumbo, ama kitu fulani. Sasa, unajua ya kwamba jambo fulani linaendelea, sivyo? Sasa, hilo halitakudhuru. Umeiona ile picha ya yule Malaika wa Bwana? Walikuwa nazo hapa wakiziuza usiku wa leo. Huyu Ndiye aliye juu yako sasa. Wewe ni...?...mwanamume. Sote wawili tuko hapa kama Wakristo tukijaribu kusaidiana. Ninajaribu kukusaidia kumpokea Yesu kama Mponyaji wako.

51 Sasa, ninamwona mwanamke, ni—ni—ni mkeo, naye ameshikilia ubavu wake, kuna shida. Una msichana mdogo, msichana mdogo ana ugonjwa wa tumbo, pia. Msichana mdogo, mwenye umri wa miaka mitatu au minne, naye ana-...Hiyo ni kweli? Uniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Nenda ukaweke

mikono yako juu ya mke wako na mtoto mchanga, nenda ukale utakacho, Yesu Kristo anakuponya. Mungu awabariki. Mungu awabariki na awe pamoja nanyi.

⁵² Unaamini—unaamini kwa moyo wako wote? Kama Mungu, bila ono, ama, atanionyesha tu shida yako, unakubali uponyaji wako? Kwanza una ugonjwa wa moyo, na jambo lingine una ugonjwa wa kike, umekuwa nao kwa muda mrefu. Unaamini ya kwamba Mungu anakuponya sasa? Unakubali uponyaji wako? Basi ondoka jukwaani ukishangilia ukisema, “Asante, Bwana Yesu.” Mungu akubariki.

⁵³ Njoo. Yuko wapi yule mama aliyeponywa sasa hivi? Mama. Mtazamishe kwangu. Angalia hapa kwa muda kidogo tu. Simama tu papo hapo kwa dakika moja tu. Shida yako ilikuwa ni nini? Uliponywa nini? Uh-huh. Hilo ni sawa. Endelea tu. Asante.

⁵⁴ Kulikuwa na mwanamke aliyesimama mbele yangu. Alikuwa . . . Sasa, una wasiwasi? Ni wasiwasi wa akili, sikuzote unafadhaika. Ibilisi amejaribu kukwambia ya kwamba ulivuka mstari wa utengano, mambo mengi, unafadhaika sana, na hasa sana jioni na alasiri. Hiyo si ni kweli? Unashikwa na wasiwasi sana, unachoka haraka sana, inakubidi kuketi chini, huwezi kusimama. Naam. Hiyo ni kweli. Ni wasiwasi. Njoo hapa. Unaamini Mungu alinipa mamlaka? Kama anaweza kumfanya kipofu aone, unaamini angeweza, tunaweza kuutoa huo kwako?

⁵⁵ Mwenyezi Mungu, ninashika mikono yake. Yeye ni mtoto Wako, dada yangu. Mrehemu.

⁵⁶ Shetani, toka ndani yake, katika Jina la Yesu Kristo, mwache mwanamke huyu!

⁵⁷ Jambo ndilo hilo, mama. Utafanya kama ninavyokwambia ufanye? Toka hapa ukiimba tu na kushangilia na kufurahi, usiwazie chochote juu yake. Amekuacha. Utakuwa mzima.

⁵⁸ Unaamini? Kwa uchaji, mkiweza, hebu kidogo. Ni vigumu sana, mnaelewa.

⁵⁹ Uko tayari kwa upasuaji, una uvimbe. Unaamini Mungu anaweza kuzuia upasuaji huo? Unaamini ya kwamba kile kinachokuzunguka sasa kinakuponya? Kinakuponya. Nenda zako tu, mshukuru Mungu kwa ajili ya uponyaji wako.

⁶⁰ Njoo, bwana. U hali gani, bwana? Ugonjwa wa moyo, jambo lingine, ugonjwa wa tumbo. Hiyo si ni kweli? Unataka kula? Unamkubali Yesu kama Mponyaji wako? Nenda ule utakacho, basi, Mungu atakuwa pamoja nawe.

⁶¹ Hapa, wakati mwanamke huyu, akija, Shetani analichochea kusanyiko. Msiwe na shaka.

⁶² Karibia kidogo tu, tafadhali, dada. Sasa, kuna kivuli cheusi. Mnamwona maskini mwanamke huyo ameketi hapo amevaa kofia nyeusi, jambo la kigeni lilikuwa likitukia wakati huo, sivyo, mama? Ulijisikia kigeni. Una shida ya kike; yeye anayo,

pia. Hiyo ni kweli? Shida ya kike. Hiyo ni kweli. Nyote wawili mmeponywa. Mungu awabariki.

⁶³ Unaamini, unapokuja? Kama Mungu atalifunua... Kama Yesu Kristo angekuwa amesimama hapa, Yeye angejua shida yako. Hiyo ni kweli? Ni ugonjwa wa damu, ninaona damu yako ikishuka chini, ni kisukari. Hiyo ni kweli? Unaamini Mungu atakuponya? Unaamini Mungu atakujaza na wema Wake, Roho Wake Mtakatifu, na kukufanya, utaishi? Nenda ukapokee zote mbili, katika Jina la Yesu Kristo. Mungu akubariki.

⁶⁴ Mungu akubariki, dada. Unaamini ulikuacha ulipopitia jukwaani? Ulikuacha. Mungu akubariki. Amina.

⁶⁵ Hebu tuseme, "Mungu na ashukuriwe." Unaamini? Kwa moyo wako wote? Je, unaamini?

⁶⁶ Hiyo hapo, papo hapo, juu ya mama huyo, tena. Naam. Ni yule mama aliye karibu naye, safu ile ile. Naam. Naam, Yeye yuko papo hapo karibu nawe, dada. Hiyo hapo ile Nuru, moja kwa moja juu yako. Simama kwa miguu yako. Unaugua ugonjwa henia ya ngiri. Unaamini Yeye anakuponya sasa? Mungu akubariki. Nenda nyumbani, na uwe mzima. Amini.

⁶⁷ Unaamini? Kidogo una shida ya kuamka, kukakamaa, yabisi kavu, na kadhalika. Hiyo ni kweli? Ulikuwa umevaa nguo zile zile. Ulikuwa ukijaribu kushuka chini hivi majuzi, kitu fulani kikakufanya kukakamaa sana hata ilikuwa vigumu kuinua mguu wako kwenye kipandio. Hiyo ni kweli? Sisomi mawazo yako, lakini hiyo ni kweli, sivyo? Vema. Imekuacha sasa. Nenda nyumbani, shangilia na umshukuru Mungu. Amina.

⁶⁸ Unamwamini Yeye?

⁶⁹ Una ugonjwa wa moyo, bwana? Unaamini Mungu alikuponya?

⁷⁰ Mungu, katika Jina la Yesu, mponye, na jalia aende nyumbani na kupata kile tu anachohitaji, katika Jina la Yesu Kristo.

⁷¹ Nenda ukishangilia. [Ndugu huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Fanya hivyo, ndugu utaponywa.

⁷² Iweni na kicho...?... Baadhi yenu katika sehemu hii anzeni kuamini. Hapa chini mahali fulani. Mtu fulani huko nyuma, huko nyuma kabisa, amini.

⁷³ Unaamini, mama? Kwa moyo wako wote? Unaamini Mungu anaweza kunifunulia shida yako ni nini? Kama anaweza, basi atakuponya. Hiyo ni kweli? Kama nikikuwekea mikono, utapona? Una yabisi kavu. Njoo hapa.

⁷⁴ Bwana, msaidie. Ninaomba ya kwamba utamponya. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponye, kwa nguvu za Mungu, ninaomba ya kwamba utamponya...?... Katika Jina la Yesu. Amina.

⁷⁵ Inua mikono yako, dada yangu, piga makofi pamoja. Sasa inua miguu yako juu chini, inua miguu yako juu chini, imetoweka. Sasa unaweza kutoka jukwaani, mzima, ukipaza sauti, ukishangilia.

⁷⁶ Hebu tuseme, “Mungu asifiwe.”

⁷⁷ Hapa. Hilo hapo tena. Kila mtu...Ninamwona msichana mdogo naye ni mdogo sana. Yeye...Ana shida, ana ninii...iko puani mwake. Huyu hapo, ana kikohozi kiletwacho na vumbi. Hiyo ni kweli? Vema, Yesu Kristo anakufanya mzima, kipenzi. Mungu akubariki.

⁷⁸ Si wewe ndiye mama yake? Hiyo ni kweli? Moyo, ugonjwa wa figo. Hiyo ni kweli? Ugonjwa wa moyo na ugonjwa wa figo. Kristo anakufanya mzima, pia, ili uweze kwenda nyumbani, uwe na furaha. Mungu akubariki.

⁷⁹ Mwaminini Mungu. Ninampa changamoto yeyote wenu kuamini!

⁸⁰ Hiyo roho ilikuwa ikimvuta. Samahani, sijachanganyikiwa, lakini mimi...kitu fulani...Ni nini ilikuwa...? Huyu msichana mdogo alikuwa wapi, ambaye ndio kwanza aponywe? Hivi yeye...? Yuko—yuko wapi? Naam. Naam, hilo ni sawa. Vema, hebu kidogo. Pepo huyo amesumbuliwa, anaita, akipiga mayowe kuomba msaada kutoka kwa wengine. Iweni na kicho. Inaonekana kana kwamba mngeweza kuiona Hiyo. Mnaiona ikijongea hapa? Ni Nuru.

⁸¹ Mama, wewe uliyeketi hapo ukiomba, una ugonjwa wa mapindi, sivyo? Naam. Nyote wawili. Hao wawili, huyo aliye karibu nawe, pia, mna mapindi. Nendeni nyumbani sasa, mkapate afya. Yesu Kristo aliwaponya. Mungu awabariki.

⁸² Amesimama karibu na huyo mama mwingine. Wako ni ugonjwa wa utumbo mpana, kwenye utumbo mpana. Hiyo ni kweli? Unakubali uponyaji wako? Anakuponya, nenda nyumbani na uwe mzima.

⁸³ Njoo, mama. Unapokuja: Unaamini? Kwa moyo wako wote? Unaniamini kuwa mimi ni mtumishi Wake? Kwa moyo wako wote? Njoo hapa kwa dakika moja. Maisha hayajakuwa rahisi sana kwako, umekuwa na shida nyingi, na hivi majuzi, pia. Ninaona mchirizi mweusi ukiambatana nawe, ukikufuata. Daima kumekuwa na shida. Wewe ni mtu mwepesi wa hasira. Daima unajenga madaraja usiyovuka kamwe, ukijitwika matatizo ya wengine. Je, hiyo ni kweli? Naam, mama.

⁸⁴ Sisomi mawazo yako, bali maisha yako, usingeweza kuyaficha, wala kitu kingine chochote humu ndani. Moja ya kasoro zako kuu sana za kimwili sasa ni ugonjwa wa tumbo. Huwezi kula kwa sababu tumbo lako limekunjamana namna *hiyo* wakati wote kutokana na hali ya wasiwasi, ilikufanya kuwa na kidonda cha tumbo. Na wakati unapoteuka chakula

chako, huyafanya meno yako kuuma sana namna hiyo. Ulidhani ilikuwa ni vijiwe-nyongo, bali sivyo, si vijiwe-nyongo, ni asidi kutoka tumboni.

⁸⁵ Ni wangapi hapa ndani walio na ugonjwa wa tumbo? Simameni kwa miguu yenu sasa hivi na mponywe pamoja na mwanamke huyu.

⁸⁶ Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao, kama maskini mtumishi Wako asiyestahili, ninakemea kila nguvu za ibilisi zinazowashikilia watu hawa. Jalia kila mmoja wa pepo hawa sasa wanaovuta hapa, hebu watoke ndani ya watu hawa. Ninawakemea wapate kuwaacha watu hawa! Jalia waende wakale, na kufurahi. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba baraka hii. Amina.

⁸⁷ Mungu awabariki. Kila mmoja wenu, nenda ukale utakacho. Wewe, pia, umeponywa sasa. Nenda ukafurahi.

⁸⁸ Nawaambia, enyi Wakristo, kamwe sijui ni upande gani. . . Kitu chote kinaonekana kama maziwa kwangu huko nje. Ni imani yenu, imani yenu ndiyo inayofanya jambo hili.

⁸⁹ Kama unaamini kuwa mimi ni mtumishi Wake, fanya kile ninachokwambia ufanye. Kubali uponyaji wako sasa hivi. Hakuna hata mmoja wenu hapa, haijalishi una shida gani, kama utasimama na kumwamini Mwana wa Mungu sasa hivi kwa ajili ya uponyaji wako, unaweza kuupokea sasa hivi. Hakika, ninasema kweli. Mungu amethibitisha kwamba ni kweli. Mnaamini? Basi hebu kila mmoja tusimame kwa miguu yetu, haidhuru una shida gani, simama, kwa vyovyote vile.

⁹⁰ Bwana, sasa ninakuomba Wewe umponye kila mmoja wa watu hawa. Roho Wako na atembe juu yao, akimkemea kila ibilisi, na jalia waponywe sasa hivi, kila mmoja wao. Ugonjwa na uondoke, na nguvu za Mungu zichukue mahali pake, kupitia Jina la Yesu Kristo. 

53-1118 Mstari wa Maombi
Evansville Coliseum
Evansville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org